**SHERIA YA KUREKEBISHA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE**

---

**MPANGILIO WA VIFUNGU**


**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Marekebisho ya sheria mbali mbali.

**SEHEMU YA PILI**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA, NAM. 2 YA 2010**

3. Kusomwa.
4. Marekebisho ya kifungu cha 5.

**SEHEMU YA TATU**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTALII ZANZIBAR, NAM. 6 YA 2009**

5. Kusomwa.
6. Marekebisho ya kifungu cha 5.
7. Kuongezwa kifungu kipya cha 5A.
8. Kuongezwa kifungu kipya cha 5B.
9. Kufutwa kwa kifungu cha 6.
10. Marekebisho ya kifungu cha 8.
11. Marekebisho ya kifungu cha 11.
12. Marekebisho ya kifungu cha 31.

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA, NAM. 12 YA 2016

13. Kusomwa.

14. Kuongezwa kifungu kipya cha 133C.

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI, NAM. 4 YA 1998

15. Kusomwa.

16. Marekebisho ya kifungu cha 3.

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA YA HIFADHI NA UENDELEZAJI MJI MKONGWE, NAM. 4 YA MWAKA 2010

17. Kusomwa.

18. Marekebisho ya kifungu cha 7.

19. Marekebisho ya kifungu cha 11.

20. Marekebisho ya kifungu cha 12.

21. Kuongezwa Sehemu mpya ya VA.

22. Marekebisho ya kifungu cha 33.

23. Marekebisho ya kifungu cha 34.

24. Marekebisho ya kifungu cha 41.

25. Marekebisho ya kifungu cha 42.

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUWAENZI VIONGOZI WA KITAIFA, NAM. 5 YA 2019

26. Kusomwa.

27. Marekebisho ya kifungu cha 2.

28, Marekebisho ya kifungu cha 4.

29. Kufutwa na kuandikwa upya kifungu cha 8.

30. Marekebisho ya kifungu cha 14.

**SHERIA NAM. 7 YA 2021**

**NIMESAINI**

{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

**24 Januari, 2022**

# SHERIA YA KUREKEBISHA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali, 2021 na itaanza kutumika mara baada ya kuwekwa saini na Rais.

Marekebisho ya sheria mbali mbali.

**2.** Sheria zilizotajwa katika sehemu mbali mbali za Sheria hii zinarekebishwa kwa namna zinavyoelezwa katika sehemu husika.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA, NAM. 2 YA 2010

Kusomwa.

**3.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Nam. 2 ya 2010, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 5.

**4.** Kifungu cha 5 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) katika kifungu kidogo cha (1) kuongeza maneno "idara, divisheni na" kabla ya neno "vitengo";

(b) kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (2) kama ifuatavyo:

"(2) Mkurugenzi, kwa kuzingatia vigezo, masharti na kwa mujibu wa Muundo wa Utumishi wa Ofisi, atateuwa wakuu wa idara, divisheni na vitengo".

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTALII ZANZIBAR, NAM. 6 YA 2009

Kusomwa.

**5.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Utalii Zanzibar, Nam. 6 ya 2009, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 5.

**6.** Kifungu cha 5 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) katika kifungu kidogo cha (1), kufuta aya ya (a) na kuweka badala yake aya mpya ya (a) na (b) kama ifuatavyo:

"(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Katibu Mtendaji".

(b) kuipa nambari mpya aya ya (b) ya kifungu kidogo cha (1) kuwa aya ya (c).

(c) kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (2) kama ifuatavyo:

"(2) Makamishna watamchagua mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti".

Kuongezwa kifungu kipya cha 5A.

**7.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 5A mara baada ya kifungu cha 5 kama ifuatavyo:

"Katibu wa vikao vya Kamisheni.

**5A.**-(1) Kamisheni itateuwa mwanasheria ambaye ni muajiriwa wa Kamisheni kuwa Katibu wa vikao vya Kamisheni.

(2) Katibu atawajibika kwa Kamisheni, na atakuwa na majukumu ya:

(a) kuchukua kumbukumbu sahihi za vikao;

(b) kutunza kumbukumbu sahihi na zinazojitosheleza;

(c) kuweka rejista la maamuzi ya vikao;

(d) kutoa taarifa sahihi za vikao;

(e) kutoa ushauri sahihi kwa Kamisheni pale unapohitajika; na

(f) kufanya kazi nyengine yoyote kama atakavyoelekezwa na Kamisheni".

Kuongezwa kifungu kipya cha 5B.

**8.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 5B mara baada ya kifungu cha 5A kama ifuatavyo:

"Muda wa Kamisheni.

**5B.** Isipokuwa mjumbe anayeingia kwa nafasi yake, Mwenyekiti na wajumbe wengine watashika nafasi kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka siku ya uteuzi na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu".

Kufutwa kwa kifungu cha 6.

**9.** Kifungu cha 6 cha Sheria Mama kinafutwa.

Marekebisho ya kifungu cha 8.

**10.** Kifungu cha 8 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta vifungu vidogo vya (2) na (3) na kuweka badala yake vifungu vidogo vipya vya (2) na (3) kama ifuatavyo:

"(2) Akidi ya kikao cha Kamisheni itakuwa zaidi ya nusu ya idadi ya Makamishna wote.

(3) Vikao vyote vya Kamisheni vitaendeshwa na Mwenyekiti na iwapo Mwenyekiti hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao".

Marekebisho ya kifungu cha 11.

**11.** Kifungu cha 11 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) kwa kufuta kifungu kidogo cha 3 (a);

(b) kwa kufuta kifungu kidogo cha 4;

Marekebisho ya kifungu cha 31.

**12.** Kifungu cha 31 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kufuta aya ya (e).

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA, NAM. 12 YA 2016

Kusomwa.

**13.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kuongezwa kifungu kipya cha 133C.

**14.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 133C mara baada ya kifungu cha 133B kama ifuatavyo:

"Utangazaji wa Misamaha katika Gazeti Rasmi.

**133C.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya sheria yoyote husika au sheria nyengine yoyote, Waziri anaweza, kwa Amri iliyochapishwa katika Gazeti Rasmi, kutangaza misamaha ya kodi yote au sehemu ya kodi, ushuru, tozo, ada au tozo nyengine yoyote.

(2) Bila ya kujali masharti ya sheria husika au sheria nyengine yoyote, Waziri anaweza, kwa Amri iliyochapishwa katika Gazeti Rasmi, kusamehe kodi yote au sehemu ya kodi, ushuru, tozo, ada au tozo nyengine yoyote kwa maslahi ya umma kama itakavyoidhinishwa na Baraza la Mapinduzi.

(3) Waziri ataweka utaratibu wa kusimamia msamaha chini ya kifungu hiki".

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI, NAM. 4 YA 1998

Kusomwa.

**15.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Nam. 4 ya 1998, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**16.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (4) kwa kufuta maneno "Hazina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania" yaliyojitokeza baina ya maneno "kwa" na "kwa mujibu wa" na kuweka badala yake maneno "Mamlaka ya Mapato Tanzania."

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA YA HIFADHI NA UENDELEZAJI MJI MKONGWE, NAM. 4 YA MWAKA 2010

Kusomwa.

**17.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe, Nam. 4 ya Mwaka 2010, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 7.

**18.** Kifungu cha 7 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongezwa aya mpya ya (g) mara baada ya aya ya (f) kama ifuatavyo:

"(g) kuruhusu uwekezaji wowote wa kibiashara, makaazi na shughuli nyengine yoyote ndani ya Mji Mkongwe wa Zanzibar kwa kuzingatia Sheria za nchi na Mpango Mkuu wa Uhifadhi na Urithi wa Mji Mkongwe";

(b) kuzipa nambari aya zilizobakia kwa mpangilio wake.

Marekebisho ya kifungu cha 11.

**19.** Kifungu cha 11 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) katika kifungu kidogo cha (1):

(i) katika aya ya (c), kufuta neno "Zanzibar" na kuweka badala yake neno "Mjini";

(ii) katika aya ya (d), kufuta neno "Nyaraka,";

(b) katika kifungu kidogo cha (3), kufuta maneno "kifungu cha10 cha Sheria ya Mitaji ya Umma" na kuweka badala yake maneno "masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma".

Marekebisho ya kifungu cha 12.

**20.** Kifungu cha 12 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongezwa aya mpya ya (e) mara baada ya aya ya (d) kama ifuatavyo:

"(e) kusimamia uendeshaji wa Mfuko wa Uhifadhi wa Mji Mkongwe".

Kuongezwa Sehemu mpya ya VA.

**21.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa Sehemu mpya ya VA mara baada ya Sehemu ya V kama ifuatavyo:

## “SEHEMU YA VA
## UANZISHWAJI WA MFUKO WA UHIFADHI WA MJI MKONGWE

Uanzishwaji wa Mfuko wa Uhifadhi wa Mji Mkongwe.

**40A.** Kunaanzishwa Mfuko wa Uhifadhi wa Mji Mkongwe utakaokuwa chini ya Bodi na kusimamiwa na Mkurugenzi Mkuu kwa mujibu wa maelekezo ya Bodi.

Madhumuni ya Mfuko.

**40B.** Madhumuni ya Mfuko ni:

(a) kukusanya fedha kutoka katika vyanzo tofauti na kuziwekeza katika uwekezaji, programu na miradi; na

(b) kuutumia Mfuko kwa ubora na ufanisi katika kuhifadhi; kuimarisha; kukarabati, na kuifanyia matengenezo miundombinu, maeneo ya kupumzikia, maeneo ya wazi na bustani ndani ya Mji Mkongwe wa Zanzibar.

Vyanzo vya Mfuko.

**40C.** Vyanzo vya Mfuko vitakuwa ni:

(a) malipo ya utangulizi yatokanayo na uwekezaji ndani ya Mji Mkongwe;

(b) ushuru utakaolipwa na watu wanaowekeza ndani ya Eneo la Urithi wa Dunia au mtu anayenufaika na huduma zilizomo ndani ya Eneo la Urithi wa Dunia;

(c) kodi ya ardhi itakayokusanywa ndani ya Eneo la Urithi wa Dunia;

(d) asilimia tano inayotokana na Mfuko wa Miundombinu wa Serikali;

(e) kodi ya majengo itakayokusanywa ndani ya Eneo la Urithi wa Dunia;

(f) ruzuku, zawadi, michango, wasia na michango mengine itakayotolewa kwa Mamlaka;

(g) mapato yatokanayo na uwekezaji uliofanywa na Mfuko;

(h) ada, faini au tozo zilizotozwa na Mamlaka; na

(i) malipo mengine yoyote halali au mali zinazopokelewa kwa ajili ya uwekezaji au uendelezaji ndani ya eneo la Mji Mkongwe wa Zanzibar.

Matumizi ya Mfuko.

**40D.** (1) Matumizi ya Mfuko yatakuwa kwa ajili ya uwekezaji, uhifadhi, uimarishaji, ukarabati, na matengenezo ya miundombinu, matengenezo **ya** majengo ya Mji Mkongwe, maeneo ya kupumzikia, maeneo ya wazi na bustani ndani ya Mji Mkongwe wa Zanzibar.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mfuko utatumika baada ya kupatikana ridhaa ya Bodi.

Taarifa na ripoti ya Akaunti ya Mfuko.

**40E.** Mfuko utakaguliwa na kutolewa taarifa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma".

Marekebisho ya kifungu cha 33.

**22.** Kifungu cha 33 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (3) kwa kuongeza maneno "anayehusika na ardhi" baina ya neno "Waziri" na "ata".

Marekebisho ya kifungu cha 34.

**23.** Kifungu cha 34 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) katika kifungu kidogo cha (1):

(i) kuongezwa maneno "anayehusika na ardhi" baina ya neno "Waziri" na neno "kuridhia";

(ii) kufuta maneno "wa Ardhi na Usajili" baina ya neno "Mkurugenzi" na "ata" na kuwekwa badala yake maneno "anayehusika na ardhi";

(b) katika kifungu kidogo cha (2), kuongezwa maneno "anayehusika na ardhi" baada ya neno "Waziri".

Marekebisho ya kifungu cha 41.

**24.** Kifungu cha 41(1) cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa.

(a) katika aya ya (a), kufuta maneno "ruzuku, zawadi, michango, wasia na michango mengine itakayotolewa kwa Mamlaka";

(b) kufuta aya ya (b);

(c) kuzipa nambari aya zilizobakia kwa mpangilio wake.

Marekebisho ya kifungu cha 42.

**25.** Kifungu cha 42 cha Sheria Mama kinarekebishwa:

(a) katika kifungu kidogo cha (1) kwa:

(i) kufuta nambari (1);

(ii) kufuta maneno "kutoka zifuatazo":

(b) kwa kufuta vifungu vidogo vya (2), (3) na (4).

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUWAENZI VIONGOZI WA KITAIFA, NAM. 5 YA 2019

Kusomwa.

**26.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, Nam. 5 ya 2019, ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**27.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa na kuandikwa upya tafsiri ya maneno "Wiki ya kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa", kama ifuatavyo:

"Wiki ya kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa Waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar na Katibu wa Kwanza wa Chama cha Afro Shirazi" maana yake ni wiki inayoanzia tarehe 1 hadi 6 Aprili ya kila mwaka.

Marekebisho ya kifungu cha 4.

**28.** Kifungu cha 4 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kuongezwa aya mpya ya (g) mara baada ya aya ya (f) kama ifuatavyo:

"(g) picha itakayoonesha sehemu ya juu ya mwili wa Marais wengine ambao wamewahi kushika nafasi ya urais wa Zanzibar na maelezo mafupi yanayoelezea vipindi vyao vya urais".

Kufutwa na kuandikwa upya kifungu cha 8.

**29.** Kifungu cha 8 cha Sheria Mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 8 kama ifuatavyo:

"Wiki ya kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, Waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar na Katibu wa Kwanza wa Chama cha Afro Shirazi.

**8.**-(1) Kutakuwa na Wiki ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, Waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar na Katibu wa Kwanza wa Chama cha Afro Shirazi kuanzia tarehe 1 hadi 6 Aprili ya kila mwaka.

(2) Wiki ya kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, Waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar na Katibu wa Kwanza wa Chama cha Afro Shirazi itajumuisha shughuli mbali mbali zenye lengo la kuwaenzi Viongozi hao.

(3) Siku ya tarehe 7 Aprili ya kila mwaka itakuwa ni siku ya Karume ambayo itakuwa ni siku ya mapumziko na Waziri, kwa kushauriana na Baraza la Mapinduzi, ataainisha pahala patakapofanyika shughuli za kumbukumbu za siku hiyo.

(4) Siku ya Karume itakuwa ni siku ya kumbukumbu ya marehemu Sheikh Abeid Amani Karume ambapo kutafanyika shughuli mbali mbali za kuashiria kukumbukwa mafanikio mazuri ya uongozi wake.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "Waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar" maana yake ni Wanzanzibari walioongoza harakati za Mapinduzi ya Zanzibar ya Mwaka 1964 chini ya uongozi wa Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Sheria hii".

Marekebisho ya kifungu cha14.

**30.** Kifungu cha 14 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (3) kwa kufuta maneno "kwa ajili ya maombolezo".

**JADWELI**
**WAASISI WA MAPINDUZI YA ZANZIBAR YA MWAKA 1964**

**[Chini ya kifungu cha 8(5)]**

---

| NAM. | JINA |
|---|---|
| 1. | KANALI MSTAAFU, MAREHEMU SEIF BAKARI OMAR |
| 2. | BRIGEDIA GENERALI MSTAAFU, MAREHEMU RAMADHAN HAJI FAKI |
| 3. | MAREHEMU MOHAMED ABDALLA KAUJORE |
| 4 | MAREHEMU SAID IDDI BAVUAI |
| 5. | MAREHEMU HAMID AMEIR ALI |
| 6. | MAREHEMU PILI KHAMIS MPERA |
| 7. | MAREHEMU SAID WASHOTO MNYUKE |
| 8 | KAMISHNA MSAIDIZI MWANDAMIZI WA POLISI MSTAAFU, MAREHEMU KHAMIS DARWESH MDINGO |
| 9. | MAREHEMU HAFIDH SULEIMAN ALMASI |
| 10. | KAMISHNA WA POLISI MSTAAFU, MAREHEMU EDDINGTON HERBERT KISSASSI |
| 11. | MEJA GENERALI MSTAAFU, MAREHEMU ABDALLA SAID NATEPE |
| 12. | MEJA GENERALI MSTAAFU, MAREHEMU YUSSUF HIMID MAFTAH |
| 13. | MAREHEMU ABDULLA MFARANYAKI |

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 22 Disemba, 2021.

..........................................
(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***